

**MTIHANI WA KAMATI YA KUIMARISHA ELIMU KATIKA WILAYA ZA
BARINGO KOIBATEK**

102/3

KISWAHILI

KARASI YA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI

SAA : 2 ½

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA: Mayai Waziri wa Maradhi

1 (LAZIMA)

Linganisha nafasi ya msichana katika Hadithi ya “Ngome ya Nafsi” na hadithi ya “Uteuzi wa Moyoni.” (alama 20)

**UTENGANO –SAID A. RIWAYA
MOHAMED**

Jibu swali la pili au la tatu

2. Said A Mohamed ameangazia migogoro na misukosuko inayosambaratisha Jumuiya ya Utengano na jamii kwa jumla. Jadili. (alama 20)
3. “Nini Bwana nimelipa mimi hapa’... moyo unamtuta macho kayatoa, anathema, kadhamiria moja tu”.
 - (a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
 - (b) elezea masaibu yaliyomkumba msemewa riwayani (alama 8)
 - (c) Taja wahusika wanne wanaoendeleza uozo wa kijamii huku ukielezea vipi (alama 8)

TAMTHILIA

KIFO KISIMANI-KITHAKA WA MBERIA

Jibu swali la nne au la tano

4. “Hatuwezi kuendelea kuwa na mwiba katika mguu wa Butangi. Butangi umo safarini. Butangi imo mbioni. Butangi inasonga mbele...”
 - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - (b) Ni mbinu zipi za sanaa zilizotumika katika dondoo hili? Taja na utue mifano miwili. (alama 2)
 - (c) Taja na ufafanue sifa Za anayezungumza (alama 10)
 - (d) eleza hatima ya anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 4)
5. Fafanua jinsi mwandishi wa Kifo Kisimani amemsawiri mwanamke (alama 20)
6. Fafanua jinsi mwandishi wa Kifo Kimani amemsawiri mwanamke (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

- | | | |
|-----|---------------------------------------|------------|
| (a) | Eleza sifa bainifu za aina za maghani | (alama 10) |
| (b) | Fafanua muundo wa vitendawili | (alama 5) |
| (c) | Ni nini dhamira ya miviga | (alama 5) |

USHAIRI

Soma mashairin yafuatayo kasha ujibu maswali.

SHAIRI A

Tunda la eleimu zote, wasema wanazuoni
Ni kwamba mtu apate, kumtambua Manani
Ndipo hadhi aipate, akumbukwe duniani.

Elimu bila ukweli, haizidi asilani
Giza na na nuru muhali, katu havitangamani
Uwongo uje kwa kweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani
Ni bora yashinda mali, taji la wanazouoni
Elimu ngema miali, iangazayo gizani.

Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni
Ulimwengu una miba, tele tele majiani
Elimu ukiishiba, u salama duniani

Wafu ni wasiosoma, watazika ardhini
Hai ndio maulama, wapaa maangani
Elimu hahari pana, milele huoni pwani

Toa wafu ujana, elimu ukitamani
Na uwe mzee sana, kujua usijihini
Elimu bahari pana, milele huoni pwani

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni
Pale uitafutapo, ujira usitamani
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
Wao wameongolewa, na ni taa duniani
Kweli wanapojua, watoe bila kuhini

Elimu bila amali, mti usio majani
Haumtii kivuli, aukaliaye chini
Inakuwa muskeli, wa kughuri insani.

SHSHAIRI B

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani
Watokao mashambani
Na kusalimu kwa bashasha
Wanaoshinda kivulini.

Chini ya mwembe
Wa umma

Inakera moyo
Hii sebule ambayo
Huwahini mezani
Wagotao nyuundo kutwa
Na kukabidhi chakula
Wanaostarehe daima

Chini ya paa
La umma;

- (a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A na B. (alama 2)
(b) haya mashairi ni ya aina gani? (alama 2)
(c) Taja sifa zozote tatu za kishairi katika shairi B (alama 3)
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa. (alama 3)
(i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika lugha nathari (alama 3)
(ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B. (alama 1)
(e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi la A katika lugha nathari (alama 3)
(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari (alama 3)
(g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A (alama 2)
(h) Eleza maana ya meneno haya kama yalivyotika katika shairi. (alama 4)
(i) Maulama
(ii) Wameongolewa
(iii) Wagotao
(iv) Huwahini.

